/ISSN 0856 – 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*No. 2* *15th January, 2026*

***SPECIAL BILL SUPPLEMENT***

*To The Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 1 Vol. 107 Dated 15th January, 2026*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

MUSWADA WA SHERIA YA MIKOPO KWA DHAMANA ZA MALI ZINAZOHAMISHIKA WA MWAKA 2026

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Fasili.

SEHEMU YA PILI
MASIJALA YA DHAMANA

4. Uanzishwaji wa Masijala.
5. Mamlaka ya Benki.

SEHEMU YA TATU
UTENGENEZWAJI WA MASLAHI KATIKA DHAMANA

6. Utengenezwaji wa maslahi katika dhamana.
7. Matumizi ya maslahi.
8. Mali zinazoweza kuwekwa dhamana.
9. Maelezo ya dhamana.
10. Mapato.
11. Mali zilizochanganywa au kubadilishwa kuwa bidhaa.

SEHEMU YA NNE
USAJILI WA MASLAHI KATIKA DHAMANA

12. Usajili wa maslahi.
13. Kipindi cha uhalali wa usajili wa maslahi.


OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA • THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

14. Maombi ya marekebisho au ufutaji wa usajili.
15. Upekuzi wa taarifa.

SEHEMU YA TANO
MASLAHI KATIKA DHAMANA DHIDI YA MTU WA TATU

16. Maslahi katika dhamana dhidi ya mtu wa tatu.
17. Maslahi katika mapato yatokanayo na dhamana dhidi ya mtu wa tatu.
18. Utekelezaji wa mali zinazoshikika zilizochanganywa dhidi ya mtu wa tatu.

SEHEMU YA SITA
VIPAUMBELE VYA MASLAHI KATIKA DHAMANA

19. Kipaumbele cha maslahi.
20. Kipaumbele kilichotengenezwa na wakopaji tofauti.
21. Kipaumbele katika mapato.
22. Kipaumbele kwa mkusanyiko wa mali au bidhaa zinazoshikika zilizochanganywa.
23. Athari za kufilisika kwa mkopaji.
24. Haki za mnunuzi, mpokeaji, mkodishaji, au mmiliki wa leseni za matumizi ya dhamana.
25. Madai ya Serikali kupewa kipaumbele.
26. Maslahi dhidi ya haki ya mshindi wa tuzo.
27. Maslahi shindani katika dhamana inayouzwa.
28. Kipaumbele dhidi ya maslahi shindani katika dhamana isiyonunuliwa.
29. Maslahi katika mapato ya dhamana inayonunuliwa.
30. Maslahi katika dhamana inayonunuliwa kwenye mali au bidhaa zinazoshikika zilizochanganywa.
31. Maslahi katika dhamana inayonunuliwa dhidi ya haki za mshinda tuzo.
32. Ubadilishaji wa kipaumbele.
33. Maslahi ya dhamana katika fedha.
34. Uhamishaji wa dhamana.

SEHEMU YA SABA
HAKI NA WAJIBU

35. Haki ya kukagua dhamana.
36. Wajibu wa kutoa taarifa.
37. Jukumu la kutunza dhamana.
38. Haki ya mdaiwa kuomba uthibitisho au kukata deni.
39. Madai ya malipo yaliyofanywa na mdaiwa wa makusanyo tarajiwa.
40. Manufaa ya mali zinazowezesha malipo au utekelezaji mwingine.
41. Haki dhidi ya taasisi inayotunza akaunti.
42. Ulinzi wa haki za mkopaji.

SEHEMU YA NANE
UTEKELEZAJI WA MASLAHI KATIKA DHAMANA

43. Matumizi ya Sehemu hii.
44. Usajili wa taarifa ya utekelezaji.
45. Uondoshaji wa dhamana.
46. Utumiaji wa dhamana kutimiza wajibu wa mkopo.
47. Utaratibu wa uondoshaji wa dhamana.
48. Taarifa ya uondoshaji wa dhamana.
49. Ukomo wa maslahi katika dhamana baada ya uondoshaji.
50. Mkopeshaji kutoa taarifa ya hesabu kwa mkopaji.
51. Mgawanyo wa mapato baada ya uondoshaji.
52. Pendekezo la kumiliki dhamana kama malipo ya deni.
53. Pingamizi dhidi ya pendekezo la kumiliki dhamana.
54. Ukomboaji wa dhamana.
55. Mkopaji kuhuisha makubaliano ya mkopo

SEHEMU YA TISA
MASHARTI YA JUMLA

56. Utekelezaji wa haki na wajibu kwa nia njema.
57. Ukiukwaji wa wajibu.
58. Kinga.
59. Utoaji wa taarifa za uongo.
60. Mapitio.
61. Rufaa.
62. Adhabu za kiutawala.
63. Adhabu ya jumla.
64. Kanuni.
65. Utambuzi wa maslahi katika Sheria ya Uhamishaji Mali.

SEHEMU YA KUMI
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI

*(a) Marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, (Sura ya 197)*

66. Ufafanuzi.
67. Marekebisho ya kifungu cha 3.
68. Marekebisho ya kifungu cha 5.

*(b) Marekebisho ya Sheria ya Kampuni, (Sura ya 212)*

69. Ufafanuzi.
70. Marekebisho ya kifungu cha 99.
71. Marekebisho ya kifungu cha 100.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · WELEDI NA UBORA · PROFESSIONALISM & EXCELLENCE · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*(c) Marekebisho ya Sheria ya Uhamishaji Mali,*
*(Sura ya 210)*


72. Ufafanuzi.
73. Marekebisho ya kifungu cha 2.
74. Kufutwa kwa kifungu cha 4.
75. Kufutwa kwa kifungu cha 24.
76. Kufutwa kwa Sehemu ya Nane na Tisa.


*(d) Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika,*
*(Sura ya 211)*


77. Ufafanuzi.
78. Marekebisho ya kifungu cha 81.
79. Marekebisho ya kifungu cha 84.


OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

## NOTISI

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni unachapishwa pamoja na maelezo ya madhumuni na sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma.

Dodoma,
14 Januari, 2026

MOSES M. KUSILUKA,
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

*Muswada*
*wa*

**Sheria ya kuweka masharti ya usimamizi wa maslahi katika dhamana za mikopo za mali zinazohamishika, kuanzisha Masijala ya usajili wa maslahi katika mali zilizotumika kama dhamana, kuainisha masharti ya utengenezaji, vipaumbele na utekelezaji wa maslahi katika dhamana, kuainisha haki na wajibu wa wahusika wa maslahi katika dhamana na masuala mengine yanayohusiana na hayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na kuanza kutumika

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2026 na itaanza kutumika kuanzia tarehe ambayo Waziri kwa Notisi, ataitangaza katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2**. Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Fasili

**3**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 197

"Benki" ina maana kama ilivyofasiliwa katika Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"bidhaa za biashara" maana yake ni mali inayoshikika inayomilikiwa na mkopaji kwa ajili ya kuuza au kukodisha kwenye biashara za mkopaji, na inajumuisha malighafi na bidhaa zilizo katika hatua ya uzalishaji;

"dhamana" maana yake ni-

(a) mali inayohamishika iliyowekwa rehani kwa ajili ya kulinda maslahi ya mkopo; au

(b) makusanyo tarajiwa ambayo maslahi yake yanaweza kuhamishwa kwenda kwa mtu mwingine;

"fedha zilizochanganywa" maana yake ni fedha kutoka vyanzo mbalimbali ambazo zimechanganywa pamoja, na kufanya kuwa vigumu kuzitenganisha;

Sura ya 197

"Gavana" ina maana kama ilivyofasiliwa katika Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"makusanyo tarajiwa" maana yake ni haki ya kulipwa deni la fedha, isipokuwa haki ya malipo inayothibitishwa kupitia hati za malipo, fedha zilizowekwa kwenye akaunti ya benki au mkopo;

"mali inayohamishika" maana yake ni mali inayoshikika au isiyoshikika ambayo inaweza kuhamishika kutoka eneo moja kwenda lingine;

"mali zilizochanganywa" maana yake ni mali zilizochanganywa kwa namna ambayo haziwezi kutambulika au kutenganishwa au kulejeshwa katika hali yake ya awali;

"mapato" maana yake ni chochote kinachopatikana kutokana na dhamana, ikijumuisha kinachopatikana kwa njia ya mauzo au namna nyingine ya uondoshaji, ukusanyaji, upangishaji, ruhusa ya kutumia dhamana, fidia ya bima, madai yanayotokana na kasoro ya kuharibika au kupotea kwa dhamana, na mapato yanayotokana na mapato ya awali;

"Masijala" maana yake ni Masijala ya Dhamana iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

"maslahi katika dhamana" maana yake ni-

(a) maslahi yanayotengenezwa kwa mkataba katika mali inayohamishika kwa lengo la kuhakikisha malipo ya mkopo; au

(b) haki ya kupokea makusanyo tarajiwa;

"maslahi katika dhamana inayonunuliwa" maana yake ni maslahi yanayotokana na mkopo wa ununuzi wa mali itakayotumika kama dhamana;

"maslahi katika dhamana isiyonunuliwa" maana yake ni maslahi ambayo yanatokana na mkataba usiohusika katika ununuzi wa mali itakayotumika kama dhamana;

"mdaiwa" maana yake ni mtu anayedaiwa malipo ya makusanyo tarajiwa ambayo yanatokana na maslahi katika dhamana, ikijumuisha mdhamini au mtu mwingine mwenye jukumu la kufanya malipo ya makusanyo tarajiwa;

"mkataba" maana yake ni makubaliano kati ya mkopaji na mkopeshaji yanayoainisha masharti ya mkopo;

"mkopaji" maana yake ni mtu ambaye anadaiwa malipo au utekelezaji wa wajibu unaolindwa na mkataba;

"mkopeshaji" maana yake ni mtu aliyesajiliwa au kupewa leseni ya kutoa mikopo kwa mujibu wa sheria; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya maslahi katika dhamana.

## SEHEMU YA PILI
## MASIJALA YA DHAMANA

Uanzishwaji wa Masijala

**4**.-(1) Inaanzishwa Masijala ndani ya Benki itakayojulikana kama Masijala ya Dhamana.

(2) Majukumu ya Masijala yatakuwa-

(a) kusajili maslahi katika dhamana;

(b) kutunza na kuhifadhi rejesta ya usajili wa maslahi katika dhamana; na

(c) kutekeleza jukumu lingine lolote linalohusiana na maslahi katika dhamana kwa namna itakavyoelekezwa na Benki.

Mamlaka ya Benki

**5**.-(1) Benki itakuwa na mamlaka ya kusimamia utendaji kazi wa Masijala.

(2) Benki inaweza, katika utekelezaji wa mamlaka yake chini ya kifungu hiki-

(a) kumtaka mtu yeyote kuwasilisha au kuthibitisha hati au nyaraka inayohusiana na suala lolote linalohusu usajili wa maslahi katika dhamana;

(b) kuelekeza taarifa yoyote au maelezo kuthibitishwa kwa kiapo; na

(c) kutoza ada ya huduma yoyote inayotolewa na Masijala.

## SEHEMU YA TATU
## UTENGENEZWAJI WA MASLAHI KATIKA DHAMANA

Utengenezwaji wa maslahi katika dhamana

**6**.-(1) Maslahi katika dhamana yatatengenezwa kwa mkataba, iwapo mkopaji ana-

(a) maslahi katika mali inayowekwa dhamana; na

(b) mamlaka ya kuweka mali hiyo dhamana.

(2) Mkataba unaweza kubainisha maslahi katika mali ya baadaye, isipokuwa kwamba maslahi hayo yatatekelezeka wakati mkopaji anapata maslahi juu ya mali hiyo na mamlaka ya kuiweka dhamana.

(3) Mkataba uliorejewa katika kifungu hiki-

(a) utakuwa kwa maandishi na utasainiwa na mkopaji na mkopeshaji;

(b) utabainisha mkopaji na mkopeshaji;

(c) utaainisha muda wa malipo ya mkopo;

(d) utabainisha kiasi cha mkopo, isipokuwa kama kuna makubaliano yanayoruhusu uhamisho wa makusanyo tarajiwa;

(e) utaainisha gharama za mkopo;

(f) utaainisha dhamana kwa kuzingatia taarifa zilizoainishwa katika kifungu cha 9; na

(g) utaainisha suala lingine lolote la msingi linalohusiana na mkopo.

(3) Utengenezaji wa maslahi katika makusanyo tarajiwa hautaathiri haki na wajibu wa mdaiwa.

Matumizi ya maslahi

**7.** Mtu mwenye maslahi katika dhamana anaweza kutumia maslahi hayo kama dhamana ya mkopo mmoja au zaidi.

Mali zinazoweza kuwekwa dhamana

**8**.-(1) Maslahi katika dhamana yanaweza kuwekwa kwenye mali inayohamishika ambayo-

(a) inashikika au isiyoshikika;
(b) ina haki zinazogawanyika au zisizoweza kugawanyika; au
(c) ina asili moja.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Gavana, baada ya kupata idhini ya Waziri, kwa Notisi katika Gazeti la Serikali atatangaza mali zinazoweza kutumika kama dhamana.

Maelezo ya dhamana

**9**. Mali iliyowekwa dhamana itabainishwa katika mkataba kwa kujumuisha taarifa zifuatazo:

(a) aina na kundi la mali;
(b) namba maalumu ya utambulisho wa mali; na
(c) kiasi, idadi au ujazo.

Mapato

**10**.-(1) Maslahi katika dhamana yatajumuisha mapato yanayotambulika yanayotokana na dhamana.

**(2)** Endapo mapato ni fedha zilizowekwa kwenye akaunti na kuchanganywa na fedha nyingine-

(a) maslahi yatajumuisha fedha zilizochanganywa, bila kujali kwamba zimepoteza utambulisho wake;
(b) maslahi katika fedha zilizochanganywa hayatajumuisha kiasi cha fedha kitakachoongezeka baada ya kuchanganywa; na
(c) ikiwa kiasi kilichochanganywa ni kidogo ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichokuwepo kabla ya kuchanganywa, maslahi katika fedha zilizochanganywa yatawekwa ukomo wa kiasi cha chini kati ya muda ambao fedha zilichanganywa na wakati ambao maslahi yatadaiwa.

Mali zilizochanganywa au kubadilishwa kuwa bidhaa

**11**.-(1) Maslahi katika dhamana-

(a) kuhusiana na mali iliyochanganywa, yatajumuisha mali zilizochanganywa; au

(b) kuhusiana na mali iliyobadilishwa kuwa bidhaa, yatajumuisha bidhaa hiyo.

(2) Maslahi katika dhamana kwa mali zilizochanganywa yatakuwa na ukomo unaolingana na thamani ya mali kabla ya kuchanganywa.

(3) Maslahi katika dhamana kwenye bidhaa yatakuwa na ukomo unaolingana na thamani ya mali kabla haijawa sehemu ya bidhaa hiyo.

## SEHEMU YA NNE
## USAJILI WA MASLAHI KATIKA DHAMANA

Usajili wa maslahi

**12**. Mkopeshaji atawasilisha Benki, maombi ya usajili wa maslahi katika dhamana kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Kipindi cha uhalali wa usajili wa maslahi

**13**.-(1) Usajili wa maslahi katika dhamana utakuwa halali-

(a) kwa kipindi chote kilichobainishwa katika mkataba;

(b) ikiwa kipindi cha utekelezaji wa mkataba hakijaisha na mkopaji ametimiza wajibu wake, kabla ya utekelezaji wa wajibu wake; au

(c) ikiwa kipindi cha utekelezaji wa mkataba kimeisha na mkopaji hajatimiza wajibu wake baada ya mkopaji kutimiza wajibu wake.

(2) Mkopeshaji anaweza kuhuisha usajili kwa kuwasilisha maombi kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Maombi ya marekebisho au ufutaji wa usajili

**14**.-(1) Mkopeshaji atawasilisha Benki maombi ya marekebisho ya taarifa kuhusiana na usajili au ufutaji wa usajili wa maslahi katika dhamana kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

(2) Maombi ya marekebisho ya taarifa yatawasilishwa, iwapo-

(a) usajili wa maslahi katika dhamana umejumuisha masuala yaliyo nje ya wigo wa mamlaka yaliyoidhinishwa kwa mkopeshaji;
(b) mkataba umerekebishwa; au
(c) kuna uhamisho wa dhamana, maslahi au sehemu ya maslahi katika dhamana.

(3) Maombi ya kufuta usajili yatawasilishwa, iwapo-

(a) usajili uliidhinishwa na mkopaji na idhini hiyo imeondolewa kwa kuzingatia masharti ya mkataba; au
(b) maslahi katika dhamana yamekoma.

(4) Mkopaji anaweza, kwa maandishi, kumtaka mkopeshaji kuwasilisha maombi ya marekebisho ya taarifa za usajili au kufuta usajili, iwapo atajiridhisha kuwa mazingira yaliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) au (3) yametokea.

(5) Endapo mkopeshaji atashindwa kutekeleza maombi chini ya kifungu kidogo cha (4) ndani ya siku kumi baada ya kupokea maombi hayo, mkopaji anaweza kuwasilisha maombi Benki kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Upekuzi wa taarifa

**15**. Mtu yeyote anaweza, baada ya kuwasilisha maombi na kulipa ada iliyoainishwa katika kanuni, kufanya upekuzi wa taarifa zilizoingizwa katika Masijala.

## SEHEMU YA TANO
## MASLAHI KATIKA DHAMANA DHIDI YA MTU WA TATU

Maslahi katika dhamana dhidi ya mtu wa tatu

**16**. Maslahi katika dhamana yatatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu iwapo yamesajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Maslahi katika mapato

**17**.-(1) Maslahi katika mapato yanayotokana na dhamana yatatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu, iwapo-

yatokanayo na dhamana dhidi ya mtu wa tatu

(a) maslahi katika dhamana yamesajiliwa; na
(b) mapato ni fedha, makusanyo tarajiwa, hati za malipo au haki ya malipo ya fedha zilizowekwa kwenye akaunti.

(2) Maslahi katika dhamana yanayohusiana na mapato ambayo hayakubainishwa wakati wa usajili, yatatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu ndani ya siku kumi za kazi baada ya kupatikana kwa mapato, isipokuwa kama kuna marekebisho ya usajili yanayohusiana na mapato hayo.

Utekelezaji wa mali zinazoshikika zilizochanganywa dhidi ya mtu wa tatu

**18.** Endapo maslahi katika mali inayoshikika yanatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu, maslahi katika mali zilizochanganywa au bidhaa ambayo maslahi hayo yamejumuishwa chini ya kifungu cha 11 yatatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu bila kuhitaji hatua zaidi.

## SEHEMU YA SITA
## VIPAUMBELE VYA MASLAHI KATIKA DHAMANA

Kipaumbele cha maslahi

**19**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, iwapo mkopaji ametengeneza maslahi zaidi ya moja katika dhamana moja, kipaumbele cha maslahi katika dhamana kitaamuliwa kwa kuzingatia tarehe na muda wa usajili.

(2) Endapo maslahi katika dhamana mbili au zaidi yanatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu, kipaumbele kitaamuliwa kwa mpangilio wa usajili, bila kujali tarehe ya utengenezaji wa maslahi katika dhamana.

(3) Kipaumbele cha maslahi kitajumuisha wajibu wote, ikiwemo wajibu ulioingiwa baada ya maslahi kuanza kutekelezeka dhidi ya mtu wa tatu.

(4) Kipaumbele cha maslahi katika dhamana kitajumuisha dhamana kama zilivyoainishwa kwenye maombi ya usajili bila kujali mkopaji alizipata kabla au baada ya usajili.

Kipaumbele kilichotengenezwa na wakopaji tofauti

**20**.-(1) Endapo mkopaji amepata dhamana ambayo maslahi yake yametengenezwa na mtu mwingine na ambayo yalianza kutekelezeka dhidi ya mtu wa tatu kabla ya mkopaji kupata dhamana hiyo, maslahi ya awali yatakuwa na kipaumbele dhidi ya maslahi yaliyotengenezwa na mkopaji katika dhamana.

(2) Kipaumbele cha maslahi ya awali katika dhamana kitaendelea kubaki kwenye dhamana baada ya kuhamishiwa kwa mkopaji mwingine, bila kujali ufahamu au ridhaa, isipokuwa kama maslahi katika dhamana yalikoma au kubadilishwa kwa mpangilio wa kipaumbele.

Kipaumbele katika mapato

**21**.-(1) Endapo maslahi katika mapato ya dhamana yanatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu, kipaumbele cha maslahi hayo kitaamuliwa kwa kutumia tarehe na muda wa usajili wa maslahi katika mali iliyozalisha mapato.

(2) Kipaumbele kilichowekwa kitaendelea kuhusiana na mapato, bila kujali aina ya mapato, ikizingatiwa kwamba-

(a) maslahi katika mali ya awali yalianza kutekelezeka dhidi ya mtu wa tatu wakati wa uondoshaji wa mali; na

(b) maslahi katika mapato yatatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu ndani ya muda uliobainishwa chini ya kifungu cha 17 (2).

(3) Masharti ya kifungu hiki hayataathiri haki za mtu wa tatu anayepata mapato kwa thamani na kwa kutofahamu uwepo wa maslahi katika dhamana, iwapo upatikanaji wa mapato hayo unalindwa chini ya Sheria hii.

Kipaumbele kwa mkusanyiko wa mali au bidhaa zinazoshikika zilizochanganywa

**22**.-(1) Endapo maslahi katika dhamana mbili au zaidi yanahusu mali zilizochanganywa kwa mkusanyiko ambazo zinashikika au zilizobadilishwa kuwa bidhaa, na kila maslahi katika dhamana yanatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu kabla ya kuchanganywa au kubadilishwa kuwa bidhaa-

(a) kipaumbele cha kila maslahi katika mali au bidhaa kitakuwa sawa na kipaumbele cha maslahi

yaliyokuwepo katika mali kabla ya kuchanganywa au kubadilishwa; na

(b) wakopeshaji watagawana mali au bidhaa kwa uwiano wa thamani ya dhamana iliyopatikana kabla ya kuchanganywa au kubadilishwa kuwa bidhaa.

(2) Thamani ya dhamana kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), itaamuliwa-

(a) kwa thamani ya soko ya kila dhamana;

(b) kwa makubaliano ya uthamini baina ya mkopeshaji na mkopaji; au

(c) na mthamini huru, ikiwa thamani ya dhamana haiwezi kuamuliwa kwa mujibu wa aya (a) na (b).

Athari za kufilisika kwa mkopaji

**23**. Maslahi katika dhamana yanayotekelezeka dhidi ya mtu wa tatu wakati mkopaji anafilisika yataendelea kuwa halali na kuendelea na kipaumbele chake, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika sheria zinazohusiana na ufilisi.

Haki za mnunuzi, mpokeaji, mkodishaji au mmiliki wa leseni za matumizi ya dhamana

**24**. Endapo dhamana imeuzwa, imehamishwa, imekodishwa, au kutolewa leseni ya matumizi wakati ambao maslahi katika dhamana yanatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu, mnunuzi, mpokeaji, mkodishaji au mtu aliyepewa leseni ya matumizi atakuwa na haki katika maslahi, isipokuwa kama-

(a) mkopeshaji ameidhinisha uondoshaji bila maslahi;

(b) mali hiyo ni mali inayoshikika na iliuzwa au kukodishwa katika utaratibu wa kawaida wa biashara wa muuzaji au mkodishaji, na mnunuzi au mkodishwaji hakuwa na ufahamu kuhusu ukiukwaji wa haki za mkopeshaji;

(c) mali hiyo ni mali isiyoshikika na ilitolewa leseni isiyotoa haki zote katika utaratibu wa kawaida wa biashara wa mtoa leseni, na mpokea leseni hakuwa na uelewa kuhusu ukiukwaji wa haki za mkopeshaji; au

(d) haki za mkodishwaji au mpokea leseni wa kwanza zimeathiriwa.

Madai ya Serikali kupewa kipaumbele

**25**. Madai ya Serikali yatokanayo na utekelezaji wa sheria nyingine kuhusiana na maslahi katika dhamana yatapewa kipaumbele dhidi ya mtu wa tatu.

Maslahi dhidi ya haki ya mshindi wa tuzo

**26**.-(1) Mshinda tuzo atakuwa na haki ya kipaumbele dhidi ya maslahi katika dhamana ikiwa amepata amri ya utekelezaji kabla ya kuanza kutekelezeka kwa maslahi dhidi ya mtu wa tatu.

(2) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) hayatatumika ikiwa tuzo inatoa umiliki wa mali inayohamishika iliyowekwa dhamana kwa mshinda tuzo.

(3) Endapo maslahi yanatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu kabla au wakati mshinda tuzo anatekeleza amri ya mahakama, maslahi yatakuwa na kipaumbele kwa kiwango cha juu cha-

(a) thamani ya mkopo uliotolewa na mkopeshaji kabla au ndani ya siku saba baada ya mkopeshaji kupokea notisi ya utekelezaji kutoka kwa mshinda tuzo; au

(b) thamani ya mkopo uliotolewa chini ya ahadi ya awali isiyoweza kubatilishwa ya kukopesha kiasi maalumu au kiasi kitakachooneshwa kwa fomula iliyotolewa kabla ya mkopeshaji kupokea notisi ya utekelezaji.

Maslahi shindani katika dhamana inayouzwa

**27**. Maslahi katika dhamana kuhusiana na muuzaji au mkodishaji yatakuwa na kipaumbele dhidi ya maslahi shindani ya mkopeshaji ambaye si muuzaji au mkodishaji.

Kipaumbele dhidi ya maslahi shindani katika dhamana isiyonunuliwa

**28.-**(1) Maslahi katika dhamana kuhusiana na ununuzi wa vifaa, bidhaa za biashara, bidhaa za matumizi au haki miliki bunifu yatakuwa na kipaumbele dhidi ya maslahi shindani katika dhamana isiyonunuliwa iliyotengenezwa na mkopaji iwapo maslahi ya dhamana yamesajiliwa.

(2) Endapo mali ni bidhaa za biashara au haki miliki bunifu inayoshikiliwa kwa ajili ya kuuzwa au kupewa leseni katika utaratibu wa kawaida wa biashara, kipaumbele cha maslahi katika dhamana inayonunuliwa kitazingatia-

(a) usajili wa maslahi katika dhamana inayonunuliwa; na
(b) utoaji wa taarifa kwa mtu mwenye maslahi katika dhamana isiyonunuliwa iliyo kwenye kundi la mali la aina moja.

(3) Maslahi katika dhamana inayonunuliwa ikiwa ni bidhaa za matumizi ya kawaida au matumizi binafsi ya haki miliki bunifu yatakuwa na kipaumbele dhidi ya maslahi shindani katika dhamana isiyonunuliwa bila kujali usajili.

Maslahi katika mapato ya dhamana inayonunuliwa

**29**.-(1) Maslahi katika mapato yatokanayo na maslahi katika dhamana inayonunuliwa yataendelea kuwa na kipaumbele sawa na maslahi katika dhamana iliyonunuliwa.

(2) Maslahi katika mapato ya dhamana inayonunuliwa kuhusiana na bidhaa za biashara au haki miliki bunifu yataendelea kuwa na kipaumbele sawa, isipokuwa kama mapato ni makusanyo tarajiwa, hati za malipo, au haki ya kulipwa kwa kupitia akaunti, ambapo, kipaumbele kitategemea taarifa ya awali iliyotolewa kwa wakopeshaji wenye maslahi shindani na usajili wa maslahi katika dhamana inayonunuliwa, kabla ya mapato kupatikana.

Maslahi katika dhamana inayonunuliwa kwenye mali au bidhaa zinazoshikika zilizochanga nywa

**30**. Maslahi katika dhamana inayonunuliwa iliyopo katika mali zinazoshikika ambayo inajumuisha bidhaa zilizochanganywa na ambayo inatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu, yatakuwa na kipaumbele dhidi ya maslahi katika dhamana isiyonunuliwa iliyotolewa na mkopaji kwenye mali zilizochanganywa.

Maslahi katika dhamana inayonunuliwa dhidi ya haki za mshinda tuzo

**31**. Maslahi katika dhamana inayonunuliwa yanayotekelezeka dhidi ya mtu wa tatu kabla ya kuisha muda ulioainishwa kwenye kifungu cha 17(2), yatakuwa na kipaumbele dhidi ya haki ya mshinda tuzo ambaye angekuwa na kipaumbele kwa mujibu wa kifungu cha 26(1).

Ubadilishaji wa kipaumbele

**32**.-(1) Mkopeshaji anaweza kubadilisha kwa kushusha kipaumbele cha maslahi yake wakati wowote kwa manufaa ya mkopeshaji mwingine mwenye maslahi shindani yaliyopo au yajayo.

(2) Ubadilishaji wa kipaumbele hautaathiri haki za mkopeshaji mwingine mwenye maslahi shindani.

Maslahi ya dhamana katika fedha

**33**. Mpokeaji wa fedha zenye maslahi atapata haki isiyofungamanishwa na maslahi hayo, isipokuwa kama mpokeaji ana ufahamu kuwa uhamisho wa fedha unakiuka haki za mkopeshaji zinazotokana na mkataba.

Uhamishaji wa dhamana

**34**. Mpokeaji wa mali isiyoshikika iliyowekwa dhamana atakuwa na haki zisizofungamanishwa na maslahi katika dhamana ikiwa amepata maslahi na kufanya malipo bila ufahamu kwamba uuzaji au uhamishaji unakiuka haki za mkopeshaji zinazotokana na mkataba.

## SEHEMU YA SABA
## HAKI NA WAJIBU

Haki ya kukagua dhamana

**35**. Mkopeshaji atakuwa na haki ya kukagua dhamana inayoshikiliwa na mkopaji au mtu mwingine.

Wajibu wa kutoa taarifa

**36.** Mkopeshaji atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa kwa mkopaji kuhusiana na mwenendo wa mkopo.

Jukumu la kutunza dhamana

**37**. Mkopeshaji au mkopaji anayeshikilia dhamana atakuwa na jukumu la kutunza dhamana hiyo.

Haki ya mdaiwa kuomba uthibitisho au kukata deni

**38**.-(1) Mdaiwa atakuwa na wajibu wa kumlipa mkopeshaji deni la mkopaji iwapo kuna uthibitisho wa maslahi ya mkopeshaji.

(2) Mdaiwa ana haki ya kutumia haki ya utetezi au haki ya kukata deni katika mkataba wa awali, iwapo haki hizo zimebainishwa katika mkataba wa awali.

Madai ya malipo yaliyofanywa na mdaiwa

**39**. Endapo mkopaji atashindwa kutimiza wajibu wa mkataba unaotengeneza makusanyo tarajiwa, mkopeshaji hatokuwa na wajibu wa kurejesha kiasi cha fedha alicholipwa na mdaiwa.

Manufaa ya mali zinazowezesha malipo au utekelezaji mwingine

**40**.-(1) Mkopeshaji mwenye maslahi katika dhamana kwenye makusanyo tarajiwa, mali au hati za malipo atanufaika na haki ya makusanyo tarajiwa, mali au hati za malipo ambazo zinawezesha au kudhamini malipo au utekelezaji mwingine wa dhamana bila hitaji la kuchukua hatua zaidi.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), iwapo haki ya makusanyo tarajiwa, mali au hati za malipo zinahamishika kwa utekelezaji mpya wa makubaliano ya uhamisho, mkopeshaji atawajibika kutekeleza masharti ya makubaliano hayo.

(3) Maslahi katika mali ambayo haki miliki bunifu imetumika hayatajumuisha haki miliki bunifu hiyo, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika mkataba.

Haki dhidi ya taasisi inayotunza akaunti

**41**.-(1) Utengenezwaji wa maslahi katika haki ya malipo ya fedha zilizowekwa kwenye akaunti-

(a) hautaathiri haki na wajibu wa taasisi inayotunza akaunti hiyo bila ridhaa ya taasisi; au
(b) hautailazimu taasisi inayotunza akaunti kutoa taarifa yoyote kuhusu akaunti hiyo kwa mtu wa tatu.

(2) Haki zote za kukata deni la taasisi inayotunza akaunti ya benki hazitaathiriwa na maslahi yoyote ambayo taasisi inaweza kuwa nayo katika haki ya malipo ya fedha zilizowekwa kwenye akaunti ya benki.

Ulinzi wa haki za Mkopaji
Sura ya 197

**42.** Ulinzi wa haki za mkopaji au utatuzi wa migogoro dhidi ya mkopeshaji utafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania.

## SEHEMU YA NANE
## UTEKELEZAJI WA MASLAHI KATIKA DHAMANA

Matumizi ya Sehemu hii

**43**. Sehemu hii haitatumika katika maslahi katika dhamana yanayotokana na uhamisho wa moja kwa moja wa makusanyo tarajiwa au ukodishaji usiofungamanishwa na utekelezaji wa masharti ya mkopo.

Usajili wa taarifa ya utekelezaji

**44**.-(1) Kabla ya kutekeleza haki katika dhamana, mkopeshaji atawasilisha Benki taarifa ya nia ya utekelezaji.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), taratibu za uwasilishaji na usajili wa taarifa ya nia ya utekelezaji zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Uondoshaji wa dhamana

**45**.-(1) Endapo mkopaji ameshindwa kutekeleza wajibu, au dhamana ipo hatarini, mkopeshaji, anaweza kuchukua hatua zozote kwa mujibu wa Sheria hii dhidi ya dhamana kwa namna ambayo haitaathiri matumizi au manufaa katika dhamana iwapo-

(a) mkopaji amekubali katika mkataba kuachilia umiliki bila amri ya mahakama; au
(b) kwa amri ya mahakama, ikiwa hakuna makubaliano.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) dhamana itakuwa hatarini iwapo mkopeshaji ana sababu za msingi za kuamini kwamba dhamana imeharibiwa au itaharibiwa, imeharibika au itaharibika, imetenganishwa au itatatenganishwa, imeondolewa au itaondolewa, imefichwa au itafichwa, imeuzwa au itauzwa, imeondoshwa au itaondoshwa kwa namna yoyote kinyume na mkataba; na
(b) kuathiri matumizi au manufaa katika dhamana kutatokea iwapo aina hiyo ya dhamana haiwezi kuondolewa kwa urahisi au hakuna sehemu inayofaa kuhifadhi dhamana hiyo.

(3) Mkopeshaji anaweza kuondosha dhamana kwa kuuza, kukodisha, kutoa leseni ya matumizi, mnada, zabuni au njia nyingine iliyoainishwa katika mkataba.

(4) Mkopeshaji anaweza kumtaka mkopaji kuwasilisha dhamana kwa ajili ya uondoshaji katika eneo alilolichagua.

(5) Mkopeshaji wakati wa uondoshaji wa dhamana iliyopo katika eneo lolote atahakikisha hakuna usumbufu usio wa lazima kwa mtumiaji wa eneo ambaye si mkopaji.

Utumiaji wa dhamana kutimiza wajibu wa mkopo

**46**.-(1) Mkopeshaji anaweza kuchukua na kutumia fedha zinazotokana na makusanyo tarajiwa, fedha au hati ya malipo iliyowekwa kama dhamana kwa ajili ya kutimiza wajibu katika mkataba ikiwa mkopaji amekiuka mkataba.

(2) Endapo mkopeshaji ana maslahi katika akaunti ya benki ya mkopaji ambayo inahusiana na mkataba, mkopaji anaweza kuielekeza taasisi ya kifedha kulipa kwa mkopeshaji kiasi cha fedha kilichopo kwenye akaunti.

Utaratibu wa uondoshaji wa dhamana

**47**.-(1) Mkopeshaji anaweza kuondosha dhamana katika hali iliyonayo au kwa namna nyingine ambayo itarahisisha uondoshaji wa dhamana hiyo.

(2) Mkopeshaji atahakikisha dhamana inaondoshwa kwa bei ya thamani ya soko.

(3) Endapo dhamana ni hati ya malipo, utaratibu wa uondoshaji wake utakuwa kwa mujibu wa sheria inayosimamia hati hizo na utahusisha mali zinazohusishwa na hati hiyo.

Taarifa ya uondoshaji wa dhamana

**48**.-(1) Mkopeshaji atatoa taarifa ndani ya siku kumi na nne kabla ya uondoshaji kufanyika kupitia fomu itakayoainishwa katika kanuni, kwa watu wafuatao:

(a) Benki;
(b) mkopaji; na

(c) mtu mwingine mwenye maslahi katika dhamana.

(2) Kifungu kidogo cha (1), hakitatumika iwapo-
(a) dhamana inaweza kuharibika kwa haraka;
(b) mkopeshaji anaamini kwamba dhamana itapungua thamani kwa kiasi kikubwa ikiwa haitauzwa kwa haraka;
(c) gharama ya matunzo na uhifadhi wa dhamana ni kubwa ikilinganishwa na thamani yake; au
(d) dhamana inajumuisha bidhaa kwa ajili ya kuuzwa, ikiwemo mazao ya kilimo au mifugo.

Ukomo wa maslahi katika dhamana baada ya uondoshaji

**49**.-(1) Endapo mkopeshaji ameondosha dhamana, maslahi yote katika dhamana hiyo, pamoja na mapato yake na haki nyingine zozote zinazotokana na dhamana hiyo, hayatawanufaisha wakopeshaji walio chini ya mkopeshaji aliyeondosha dhamana.

(2) Endapo dhamana imeondoshwa, mkopeshaji atawasilisha maombi ya ufutaji usajili Benki kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Mkopeshaji kutoa taarifa ya hesabu kwa mkopaji

**50**. Mkopeshaji, baada ya uondoshaji wa dhamana, atatoa taarifa ya hesabu kwa maandishi kwa watu walioorodheshwa katika kifungu cha 48(1), kwa kuzingatia utaratibu utakaobainishwa katika kanuni.

Mgawanyo wa mapato baada ya uondoshaji

**51**.-(1) Mkopeshaji ambaye ameondosha dhamana atatumia mapato ya uondoshaji ili kulipa deni la mkopaji linalotokana na mkataba.

(2) Endapo mkopeshaji ameondosha au amebakisha dhamana kwa ajili ya kukidhi deni, mkopeshaji atalipa bakaa kwa mtiririko ufuatao:
(a) wakopeshaji wengine kwa mujibu wa mpangilio wa vipaumbele vyao; na
(b) mkopaji.

(3) Endapo kuna mgogoro kuhusiana na mtu anayestahili kupokea malipo, mkopeshaji anaweza kulipa bakaa mahakamani.

(4) Mkopaji, kwa madhumuni ya kukidhi deni, atawajibika kulipa kiasi chochote cha deni kinachodaiwa baada ya uondoshaji wa dhamana.

Pendekezo la kumiliki dhamana kama malipo ya deni

**52**.-(1) Endapo mkopaji ameshindwa kutimiza wajibu wa mkataba, mkopeshaji anaweza kupendekeza kumiliki dhamana kama malipo ya deni kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

(2) Mkopeshaji atatoa taarifa ya maandishi ya nia ya kumiliki dhamana kwa Benki na mmiliki wa mali.

Pingamizi dhidi ya pendekezo la kumiliki dhamana

**53**.-(1) Mtu ambaye amepokea taarifa ya pendekezo la mkopeshaji kumiliki dhamana na ambaye maslahi yake katika dhamana yanaweza kuathiriwa ikiwa mkopeshaji atamiliki dhamana hiyo, atawasilisha Benki taarifa ya maandishi ya pingamizi la pendekezo ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa ya pendekezo hilo.

(2) Utaratibu wa kuwasilisha na kusikiliza pingamizi utakuwa kama utakavyoainishwa katika kanuni.

Ukomboaji wa dhamana

**54**.-(1) Wakati wowote, kabla ya mkopeshaji kuondosha dhamana au kumiliki dhamana ili kukidhi deni, mkopaji au mkopeshaji mwingine anaweza kukomboa dhamana kwa-

(a) kutimiza wajibu wote unaolindwa na dhamana; na

(b) kulipa gharama nyingine stahiki alizotumia mkopeshaji kuhusiana na dhamana husika.

(2) Haki ya mkopaji ya kukomboa dhamana itapewa kipaumbele dhidi ya haki ya mtu mwingine.

Mkopaji kuhuisha makubaliano ya mkopo

**55**. Mkopaji anaweza, kwa makubaliano na mkopeshaji, kuhuisha mkopo wakati wowote kabla ya mkopeshaji kuondosha au kumiliki dhamana kama malipo ya deni.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI YA JUMLA

Utekelezaji wa haki na wajibu kwa nia njema

**56**. Haki na wajibu unaotokana na mkataba au Sheria hii utatekelezwa kwa nia njema na kwa viwango stahiki vya uadilifu kibiashara.

Ukiukwaji wa wajibu

**57**.-(1) Endapo mkopeshaji atashindwa kutekeleza jukumu lolote au wajibu uliowekwa na Sheria hii, mtu ambaye jukumu hilo au wajibu huo unatekelezwa dhidi yake, pamoja na mtu mwingine yeyote ambaye anategemea utekelezaji wa jukumu hilo au wajibu huo, atakuwa na haki ya kudai fidia ya hasara au uharibifu wowote uliotokea kutokana na kushindwa kutekeleza jukumu au wajibu huo.

(2) Masharti ya kifungu hiki hayatazuia au kuathiri uwajibikaji wowote alio nao mtu chini ya sheria nyingine.

Kinga

**58**. Mtu hatawajibika kwa kitendo chochote kilichosababisha madhara au kwa kutofanyika katika utekelezaji wa mamlaka au jukumu alilopewa au lililowekwa kuwezesha utekelezaji chini ya Sheria hii, isipokuwa kama kitendo au kutofanyika kwa kitendo kulikua kwa nia ovu au uzembe.

Utoaji wa taarifa za uongo

**59**. Mtu ambaye-

(a) anaingiza au anawezesha kuingizwa kwa taarifa za uongo katika Masijala; au

(b) anatoa au kutumia taarifa za uongo au za kughushi kuhusu usajili,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote.

Mapitio

**60**. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Benki anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio kwa Benki kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Rufaa

**61**.-(1) Mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Benki baada ya mapitio, anaweza kwa maandishi, ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokea taarifa ya uamuzi, kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Waziri ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokea rufaa, atatoa uamuzi wa rufaa.

Adhabu za kiutawala

**62**.-(1) Mkopeshaji atachukuliwa kuwa ametenda kosa la kiutawala, iwapo-
(a) hajawasilisha maombi ya usajili wa maslahi, marekebisho ya usajili au ufutaji wa usajili; au
(b) hajatekeleza maelekezo yaliyotolewa na Benki.

(2) Endapo mkopeshaji ametenda kosa la kiutawala, Benki inaweza kutoa adhabu zifuatazo:
(a) onyo kwa njia ya maandishi; au
(b) faini isiyozidi asilimia 10 ya thamani ya maslahi katika dhamana.

(3) Gavana atatengeneza kanuni zitakazoweka utaratibu wa utekelezaji wa adhabu za kiutawala.

Adhabu ya jumla

**63**. Mtu anayekiuka masharti ya Sheria hii au kanuni zitakazotengenezwa chini yake ambayo hakuna adhabu mahususi iliyoainishwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote.

Kanuni

**64**.-(1) Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kutengeneza kanuni kuhusu-
(a) taratibu za usajili wa maslahi katika dhamana;
(b) taratibu za utoaji na uwasilishaji wa nyaraka;
(c) taratibu za kuwasilisha na kushughulikia pingamizi;

(d) ada na tozo;
(e) taratibu za kuwasilisha maombi ya mapitio na rufaa; au
(f) suala lolote litakalowezesha utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Utambuzi wa maslahi katika Sheria ya Uhamishaji Mali Sura ya 210

**65**. Usajili wowote wa maslahi katika dhamana uliofanyika chini ya Sheria ya Uhamishaji Mali utachukuliwa kuwa umefanyika chini ya Sheria hii na utaendelea kutekelezwa chini ya Sheria hii hadi kufikia ukomo wake.

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI

*(a) Marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, (Sura ya 197)*

Ufafanuzi Sura ya 197

**66**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ambayo hapa inarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 3

**67**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 3, kwa kuongeza katika mpangilio wa kialfabeti fasili ya msamiati ufuatao:

""Collateral Registry" means the registry established as such under the Secured Transactions Act;""

Marekebisho ya kifungu cha 5

**68**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 5(1) kwa kuongeza maneno ", administer collateral registry" mara baada ya neno "Tanzania".

*(b) Marekebisho ya Sheria ya Kampuni, (Sura ya 212)*

Ufafanuzi Sura ya 212

**69**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kampuni, ambayo hapa inarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu 99

**70**. Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 99 na kukiandika upya kama ifuatavyo:

"""Registration of charges

**99**.-(1) Where a company creates a charge, the charge, in so far as any security on the property or undertaking of the company is conferred by it, is void against-

(a) a liquidator of the company;

(b) an administrator of the company; and

(c) a creditor of the company,

unless the requirements under the law governing secured transactions on movable properties have been complied with.

(2) A company that creates a charge shall ensure that particulars of a charge together with the instrument if any, by which the charge is created or evidenced are, delivered to the Registrar for registration.

(3) The particulars under subsection (2) shall be delivered for registration within forty two days from the date upon which the charge became effective against third parties in accordance with the requirement of the applicable laws of the charge.

(4) This section shall not affect any contract or obligation for repayment of the money thereby secured, and where a

charge becomes void under this section, the money secured thereby shall immediately become payable.”.

Marekebisho ya kifungu cha 100

**71**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 100(5) kwa kuongeza maneno “or security interest as defined under the Secured Transactions Act” mara baada ya neno “mortgage” lililopo katika aya (a).

*(c) Marekebisho ya Sheria ya Uhamishaji Mali, (Sura ya 210)*

Ufafanuzi Sura ya 212

**72**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Uhamishaji Mali, ambayo hapa inarejewa kama “Sheria kuu”.

Marekebisho ya kifungu cha 2

**73**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 2 -

(a) katika fasili ya kwanza ya msamiati “instrument” kwa kufuta maneno, “mortgage, lien”; na

(b) katika fasili ya pili ya msamiati “instrument” kwa kuongeza mara baada ya aya (n), aya ifuatayo:

“(o) mortgage or any other form of lien under the Secured Transactions Act.”.

Kufutwa kwa kifungu cha 4

**74.** Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 4.

Kufutwa kwa kifungu cha 24

**75.** Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 24.

Kufutwa kwa Sehemu ya Nane na Tisa

**76.** Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta Sehemu ya Nane na Sehemu ya Tisa mtawalia.

*(d) Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, (Sura ya 211)*

Ufafanuzi
Sura ya 211

**77**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Vyama vya Ushirika, ambayo hapa inarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 81

**78**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 81-

(a) kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kukiandika upya kama ifuatavyo:

"(2) Where a registered society creates a charge, the charge shall, in so far as any security on the society's property is thereby conferred, be void against the liquidator and any creditor of the society unless the requirements under the law governing secured transaction of movable properties have been complied with.";

(b) kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (2) yafuatayo:

""(3) A cooperative society that creates a charge shall ensure that particulars of a charge, together with the instrument if any, by which the charge is created or evidenced are delivered to the Registrar for registration within thirty days after the date upon which the charge became effective against third parties.

(4) This section shall not affect any contract or obligation for repayment of the money thereby secured, and where a charge becomes void under this section, the money secured thereby shall immediately become payable."";

(c) kwa kupangilia upya vifungu vidogo vya (3), (4), (5), (6) na (7) kama vifungu vidogo vya (5), (6), (7), (8) na (9) mtawalia;

(d) katika kifungu kidogo cha (5) kama kilivyopangiliwa upya kwa kufuta maneno

"Chattels Tranfer Act" yaliyopo katika aya (b) na badala yake kuweka maneno "Secured Transactions Act";

(e) katika kifungu kidogo cha (8) kama kilivyopangiliwa upya kwa-

(i) kufuta maneno "the execution of the deed containing the charge, or, if there is no deed after the execution of any debentures of the series," yaliyopo katika maneno ya ufunguzi na badala yake kuweka maneno "the date upon which the charge or debentures of the series became effective against third parties in accordance with the requirements under the law governing secured transaction of movable properties";.

(ii) kuongeza mara baada ya aya (b) aya mpya ifuatayo:

"(c) proof of registration of the charge or debentures in accordance with with the requirements under the law governing secured transaction of movable properties;"; na

(iii) kupangilia upya aya (c) na (d) kama aya (d) na (e) mtawalia.

Marekebisho ya kifungu cha 84

**79**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 84(1)-

(a) kwa kufuta aya (b);

(b) kwa kupangilia upya aya (c) kama aya (b);

(c) katika aya (b) kama ilivyopangiliwa upya kwa-

(i) kuongeza mara baada ya aya ndogo ya (i) yafuatayo:

"(ii) proof of registration of the charge in accordance with the requirements under the law governing secured transaction of movable properties;"; na

(ii) kupangilia upya aya ndogo za (ii), (iii) na (iv) kama aya ndogo za (iii), (iv) na (v) mtawalia.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana ya Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2026 kwa lengo la kuweka masharti ya usimamizi wa maslahi katika dhamana za mikopo za mali zinazohamishika, kuanzisha Masijala ya usajili wa maslahi katika mali zilizotumika kama dhamana, kuainisha masharti ya utengenezaji, vipaumbele na utekelezaji wa maslahi katika dhamana, kuainisha haki na wajibu wa wahusika wa maslahi katika dhamana, kuweka udhibiti wa vihatarishi vinavyotokana na usajili wa maslahi katika dhamana za mali zinazohamishika na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Serikali kwa kutambua umuhimu wa maendeleo ya sekta ya fedha katika ukuaji wa uchumi wa Taifa iliandaa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21 hadi 2029/30 sambamba na Mkakati wa Upatikanaji wa Huduma Jumuishi za Fedha 2023-2028 na Mkakati wa Upatikanaji wa Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo na Wa Kati wa mwaka 2023/24 - 28/29 ikiwa na lengo la kutambua umuhimu wa uendelezaji wa sekta ya fedha. Pamoja na uwepo wa mikakati na mipango ya Serikali katika kuboresha na kukuza sekta ya fedha, usimamizi, usajili wa mali zinazohamishika pamoja na utoaji mikopo unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210, Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura ya 117, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211, Sheria ya Mikopo ya Fedha, Sura ya 417, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sura ya 407. Hata hivyo, changamoto zilizobainika katika sheria hizo ni kutokuwepo kwa masijala jumuishi inayohusiana na usajili wa maslahi katika dhamana zinazohamishika, kutokuwa na sheria mahsusi ya kusajili maslahi katika dhamana katika mali zinazohamishika na kutokuwepo kwa utaratibu wa udhibiti wa vihatarishi vinavyotokana na maslahi katika dhamana suala ambalo limepelekea taasisi za fedha na wakopeshaji kushindwa kutumia mali hizo kama dhamana wakati wa ukopeshaji.

Kwa msingi huo, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya kusimamia mikopo kwa dhamana za mali zinazohamishika. Lengo ni

kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wananchi hivyo, kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Aidha, Muswada unaopendekezwa unakusudia kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali ikijumuisha Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 na Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Kumi. Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya Utangulizi, yanayobainisha jina la Sheria, utaratibu wa kuainisha tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa kutungwa na fasili ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu Masijala ya Dhamana. Sehemu hii inajumuisha masharti kuhusu uanzishwaji wa Masijala ya Dhamana chini ya Benki Kuu ya Tanzania itakayohusika na kusajili maslahi katika dhamana kwa mali zinazohamishika, kutunza na kuhifadhi rejesta za usajili wa maslahi katika dhamana na kufanya majukumu mengine yanayohusiana na hayo. Aidha, Benki Kuu itakuwa na mamlaka ya kutoza ada za usajili pamoja na huduma nyinginezo.

Sehemu ya Tatu inahusu utengenezwaji wa maslahi katika dhamana. Sehemu hii, inajumuisha masharti ya msingi katika mkataba wa mkopo na masharti ya matumizi ya maslahi katika deni moja au zaidi. Aidha, Sehemu hii inaainisha mali zinazoweza kuwekwa dhamana, ikiwa ni pamoja na mali zinazoshikika na zisizoshikika, mali zenye haki zinazoweza au zisizoweza kugawika au mali zenye asili moja. Aidha, inaweka masharti kuhusu mapato yanayotokana na dhamana, ikiwemo fedha, mali zilizochanganywa au bidhaa zilizoundwa pamoja na mipaka ya maslahi katika mali hizo.

Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu usajili wa maslahi katika dhamana. Sehemu hii, inaainisha wajibu wa mkopeshaji kuwasilisha notisi ya maslahi kwa Benki kwa ajili ya usajili. Vilevile, Sehemu hii inabainisha masharti kuhusu kipindi cha uhalali wa usajili, marekebisho ya usajili kabla ya kuisha muda wake na masharti kuhusu kufuta usajili. Aidha, Sehemu hii inaruhusu mtu yeyote kufanya upekuzi wa taarifa zilizosajiliwa katika Masijala.

Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu maslahi katika dhamana dhidi ya mtu wa tatu. Sehemu hii, inaainisha masharti kuhusu maslahi katika dhamana kuwa na nguvu ya kutekelezeka dhidi ya mtu wa tatu iwapo maslahi hayo yatasajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii. Aidha, Sehemu hii inabainisha utekelezekaji wa maslahi katika mapato yatokanayo na dhamana. Vilevile, Sehemu hii inaweka masharti kuhusu utekelezekaji wa maslahi katika mali zinazoshikika zilizochanganywa au kubadilishwa kuwa bidhaa.

Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu vipaumbele vya maslahi katika dhamana. Sehemu hii, inaainisha masharti kuhusu vipaumbele vya kuzingatia iwapo kuna maslahi zaidi ya moja katika dhamana au dhamana zinazofanana. Aidha, Sehemu hii inaainisha vipaumbele vya maslahi vilivyotengenezwa na wakopaji tofauti, maslahi katika mapato, mali zilizochanganywa au kubadilishwa kuwa bidhaa na athari za kufilisika kwa mkopaji. Vilevile, Sehemu hii imeweka masharti kuhusu haki za wanunuzi, wapokeaji, wakodishaji na watu waliopewa leseni, na kubainisha kipaumbele kwa madai ya Serikali. Aidha, Sehemu hii imebainisha misingi ya kuzingatia wakati wa kuamua vipaumbele.

Sehemu ya Saba ya Muswada inaainisha haki mbalimbali na wajibu wa watu wenye maslahi katika dhamana ikiwemo wajibu wa mkopeshaji kukagua dhamana pamoja na haki ya mkopaji kupata taarifa muhimu kuhusu mwenendo wa deni, wajibu wa mtu anayeshikilia dhamana, haki za mdaiwa kuomba uthibitisho au kukata deni, haki ya madai ya malipo kuhusiana na makusanyo tarajiwa, haki za mali za wahusika, haki dhidi ya taasisi na ulinzi wa haki za mkopaji.

Sehemu ya Nane ya Muswada inaainisha utekelezaji wa maslahi katika dhamana. Sehemu hii, inaweka ukomo na vigezo vya matumizi ya maslahi yanayotokana na uhamisho wa moja kwa moja. Aidha, Sehemu hii inabainisha masharti kuhusu usajili wa taarifa ya nia ya utekelezaji, ushikiliaji au uondoshaji wa dhamana, utumiaji wa dhamana kutimiza wajibu wa mkopo, utaratibu wa uondoshaji wa dhamana, ukomo wa maslahi baada ya uondoshaji, hitaji la kutoa taarifa kwa mkopaji, mgawanyo wa mapato, umiliki wa dhamana kama malipo ya deni, haki ya pingamizi kwenye dhamana, ukomboaji wa dhamana na makubalino ya kuhuisha mkopo.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inaweka masharti ya jumla. Sehemu hii inajumuisha hitaji la utekelezaji wa haki na wajibu kwa nia njema, makosa na adhabu, mapitio, rufaa, mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni, pamoja na masharti ya mpito na mwendelezo.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inajumuisha marekebisho katika sheria mbalimbali ili kuendana na masharti yanayopendekezwa katika Sheria hii. Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210 na Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211. Aidha, marekebisho katika sheria hizo yanaweka masharti ya utambulisho wa nyaraka na masharti ya kusajiliwa kwa maslahi au dhamana ili kulinda haki za wahusika na kuhakikisha utekelezaji bora wa Sheria ya Mikopo ya Dhamana kwa Mali Zinazohamishika.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA • WELEDI NA UBORA • PROFESSIONALISM & EXCELLENCE • THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

Dodoma,
12 Januari, 2026

KHAMIS MUSSA OMAR,
*Waziri wa Fedha*